**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

Simu: +255 26 2322761-5
Fax No. +255 26 2324218
E-mail: **cna@bunge.go.tz**

Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S. L. P. 941,
40490 Tambukareli,
**DODOMA.**

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KUANZA KWA VIKAO VYA KAMATI ZA BUNGE

---

Vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge vitaanza kufanyika siku ya Jumanne tarehe 13 hadi Ijumaa tarehe 23 Januari, 2026 katika Ofisi ya Bunge Jijini Dodoma. Vikao hivi ni kwa ajili ya maandalizi ya Mkutano wa Pili wa Bunge unaotarajiwa kuanza siku ya Jumanne, tarehe 27 Januari, 2026. Kufuatia ratiba hiyo Waheshimiwa Wabunge wanatakiwa kufika Dodoma siku ya Jumatatu, tarehe 12 Januari, 2026.

Shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Kamati za Bunge katika kipindi hicho ni kama ifuatavyo:-

a) Uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kwa mujibu wa Kanuni ya 138(11) ya Kanuni za Bunge za Mwaka 2025;
b) Kamati kuzifahamu Wizara na Taasisi zake na baadhi ya Sera na Sheria kulingana na majukumu ya kila Kamati kama ilivyofafanuliwa kwenye Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge chini ya Kanuni ya 140 ya Kanuni za Bunge;
c) Kamati kupitishwa kwenye majukumu yake ya msingi; na
d) Kamati ya Bajeti kufanya maandalizi ya Hoja zitakazojadiliwa na Bunge.

Ratiba ya shughuli za Kamati inapatikana katika tovuti ya Bunge ambayo ni www.bunge.go.tz

**Imetolewa na :** Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma
Ofisi ya Bunge
**Dodoma**

6 Januari, 2026